

NTAPATA BILA AJIZI

1. Sintojali ukosefu, iwapo hapana budi,
Ijapokuwa mrefu, wa adha na nyingi tadi,
Ntatundama pasi hofu, kwa nguvu kama hadidi,
Kuna siku ya idadi. Ntapata bila ajizi.
2. Kukosa ulainifu, na yabisi kuja hodi,
Kwa hilo ni maarufu, huwaje kuniradidi,
Dunia mti mkafu, hutashika usfadi,
Kwa kuzidi maradufu. Ntapata bila ajizi.
3. Kushika na kujisifu, pasi hofu ya baridi,
Mie sasa kwanikifu, si kasidi si kasidi,
Nenda utoe uchafu, si mzia maridadi,
Itatimia ahadi. Ntapata bila ajizi.
4. Kumuiga mausufu, bado sijaweka hadi,
Japo nikanywe kwa ngufu, sintaliwaa mradi,
Hata akimbie kufu, si tayari kurutadi,
Atazidisha Raufu. Ntapata bila ajizi.
5. Aaini kwa mikufu, na vitu bora zaidi,
Ili kunitia hofu, madhara kama abidi,
Sintoviacha vichafu, japo nguvu inizidi,
Hata na visivyofidi. Ntapata bila ajizi.
6. Kusilikwa kwa utomfu, naona hainibidi,
Hata kufika Raufu, hakuhadi hakuhadi,
Katu sintaumwa mafu, huonakwe ni jadidi,
Na hayo yalo nafuu. Ntapata bila ajizi.

Hamidu R. Tambwe
MBEYA, Tanzania 26/07/1970.
